World Council of Churches

# Upendo wa Kristo Unauleta Ulimwengu katika Umoja na Upatanisho

## Tafakuri juu ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa 11 wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni, Karlsruhe 2022

Mwaka 2022, Baraza la Makanisa Ulimwenguni litafanya mkutano mkuu mjini Karlsruhe, Ujerumani. Mikutano mikuu hii ni wasaa ambapo makanisa ndani ya ushirika wa WCC, yakiitikia wito wa Kristo “kwamba wawe na umoja kamili” (Yohana 17:23), yakialikana mmoja mmoja katika umoja unaoonekana kwa ajili ya ulimwengu ambao Mungu anaupenda na kwa ajili ya uumbaji ambao Mungu anatangaza kuwa ni mwema.



Picha: Albin Hillert/WCC

# Muktadha ambapo tutakutana

Mkutano Mkuu wa 11 utafanyika katikati ya Ulaya, mjini Karlsruhe, Ujerumani, nchi yenye utajiri mkubwa lakini, kama zilivyo nchi nyingi zilizokumbwa na athari ya Uviko-19 katika ustawi wa watu: kwa mtu binafsi, kiuchumi na kiroho.

Mkutano huu utakuja baada ya kusitishwa kwa muda kwa sababu ya janga lililoikumba dunia, virusi hivi vimeonesha na kudhihirisha udhaifu wa binadamu na namna alivyo rahisi kudhurika pamoja na namna tulivyogawanyika na kukosekana usawa kati yetu. Ulimwengu umeamshwa na kuoneshwa ukweli wa dhati wa uwepo wa upendeleo na ukandamizaji wa kiuchumi, kijamii na udhalimu wa kikabila.

Kutokana na uzoefu huu, makanisa kwa kutii maagizo ya Mungu yatakutana pamoja ili kupokea nuru ya tumaini na kusherehekea upendo wa Mungu Utatu Mtakatifu, upendo uliodhihirishwa kikamilifu katika Yesu Kristo ambao unawaleta watu katika umoja na upatanisho . Katika nyakati tunazoishi sasa, tutajiuliza kila mmoja, “Ni kwa jinsi gani kanisa, ambamo upendo wa Kristo unafurahia kuwepo, linapanga, linazungumza na kutenda katika majira haya?” na “Kwa jinsi gani wakati huu, tunaweza kushiriki pamoja katika utume wa Mungu wa upendo kwa ulimwengu?”


Picha: Albin Hillert/WCC

Kuanzia mwaka 2013, wito wa pamoja katika makanisa umeelezewa kama hija ya haki na amani, na kutakuwa na mambo mengi ya kukumbukwa na kusherehekewa kwa furaha kadiri tunavyotafakari kuhusu yote ambayo yametokea katika kutembea kwetu pamoja tangu hapo. Mkutano huu pia utakuwa ni muda wa kupata hamasa kwa ajili ya hatua za safari zinazofuata, hatua zinazopaswa kuchukuliwa chini ya bendera ya upendo wa Mungu, Utatu Mtakatifu; upendo uliofunuliwa katika Kristo na kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu, upendo unaoingia na kupitia wanadamu wote na viumbe wote.

Janga la ugonjwa duniani kote limechukua maisha ya watu wengi na limeleta changamoto kubwa kuhusu utaratibu wa maisha ambao wengi wameuchukulia kama "kawaida." Katika kukabiliana na janga na kifo, tumetambua upya umuhimu wa kutegemeana baina yetu, ukomo wa ubinafsi, changamoto za utandawazi (ambazo zinawezesha kusambaa kwa virusi kwa haraka), na wajibu wetu wa pamoja kwa kila mmoja wate (na wakati mwingine pia kila mmoja kumhofu mwenzake).

Wakati huo huo, vita na umasikini unaendelea kuleta shida nyingi, mateso na kifo. Mabadiliko ya tabianchi, ambayo hayakuzingatiwa na wengi kwa miongo kadhaa, sasa yanaleta kiwango kipya cha hofu miongoni mwa baadhi ya watu, na tayari yanaleta maafa na tishio kwa watu masikini zaidi duniani. Siasa zinabadilika haraka, katika jumuiya tajiri na masikini, aidha, demokrasia yenyewe, kwa baadhi ya watu, inaonekana imechoka na mara nyingi inakuwa ni ahadi hewa. Majukwaa yanayohusisha pande nyingi na michakato ya kufanya uamuzi wa pamoja katika ngazi ya kimataifa inafifia haraka sana na wakati mwingine husahauliwa tunapokabiliana na majanga mkubwa.

Wale walio ndani ya Kristo, wanaouishi upendo wa Kristo unaofanya kazi ndani yetu, wanahimizwa kufanya hivyo katika dunia hii, kuwa jumuiya inayotazama maisha ya siku za mwisho (kieskatolojia), wakiishi kama ishara na alama ya ufalme ujao na kuudhihirisha upendo ambao unajaza mioyo yetu kwa furaha hata katika siku za taabu sana.

Mkutano huu utakuwa ni muda wa kukusanya nguvu kwa ajili ya hija yetu ya pamoja hapa ulimwenguni katika uhalisia wake wa sasa, kumsikiliza kila mmoja, na kutiana moyo tunapofurahia upendo ambao kupitia Roho Mtakatifu, unatuongoza, unatuponya na kututia nguvu.

Pamoja, tukiwa tumezama katika upendo kwa ajili ya Kristo, tukiimarishwa na Roho Mtakatifu, na kuinuliwa na Mungu aliye asili ya uhai wetu na uumbaji wote, ushirika wa makanisa utapata nguvu kwa ajili ya safari na matumaini kwa ajili ya wakati ujao. Tutatafuta njia za kuwahudumia wale ambao wanaamini hawapendwi, wamepuuzwai na hawaonwi na kuleta upendo wa Mungu kwa waliopotea, upatanisho kwa wale walio katika mgogoro na umoja kwa wale waliofarakana kwa wakati mmoja tunapofurahia kupokea zawadi na baraka sisi wenyewe.



Picha: Albin Hillert/WCC

# *“Upendo wa Kristo . . . ”*

## Misingi ya kibiblia na kiteolojia kuhusu ujumbe huu

Ujumbe “upendo wa Kristo unauleta ulimwengu katika umoja na upatanisho “ umehamasishwa moja kwa moja na 2 Wakorintho 5:14[1] na unatoka katika kitovu halisi cha injili inayoupatia ulimwengu maajabu na kina cha upendo wa Mungu Utatu Mtakatifu. Unatokana na mpango wa Mungu kwa ajili ya umoja na upatanisho wa wote, mpango ambao uliwekwa wazi kwa Mungu kufanyika mwili kupitia upendo wa Mungu kwa Yesu Kristo.

Kwa Paulo, ambaye aliwaandikia Wakristo wa Korintho, Yesu Kristo si tu mwalimu wa Galilaya au mwanzilishi wa dini mpya na ya kipekee, bali Kristo wa malimwengu yote ambaye katika yeye “unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya kimwili” (Kol. 2:9). Kutokana na upendo kwa ajili yetu na kwa viumbe wote, Mungu akafanyika mwili, akapata mateso na maumivu yote ya wanadamu na ya uumbaji wake wote ili atuponye, aturejeshe, atuokoe, na atupatanishe na Mungu. Imani yetu inatuambia kwamba “Mungu ni upendo” (1 Yohana 4:16) na kwamba, katika Yesu Kristo, upendo huu wa Mungu umejidhihirisha kwa ulimwengu.

Kama ambavyo Neno lilifanyika mwili katika Yesu Kristo, hivyo tumeitwa ili tuwe “ndani ya Kristo” na kuishi na Kristo kwa upendo wa Mungu ambaye ni mtakatifu na wa milele. Kanisa, kama mwili wa Kristo (Efe. 1:22-23), hupokea, huishi, hushuhudia na kuueneza upendo huo kwa wengine ili kwamba amani, haki na umoja uonekane katika maeneo yote ambapo watoto wa Mungu sasa wanalia kutokana na mateso yao na katika maeneo ya uonevu na fujo.

---

1 2 Wakorintho 5:14a: “Maana upendo wa Kristo watubidisha. . . ”

Ujumbe wa mkutano wowote huweka msingi kwa ajili yakusanyiko la ushirika na hutoa  picha ya maisha yetu na safari yetu pamoja na kuweka mwelekeo wa safari zijazo. Inakuwa ni njia yenye ufanisi kwa ajili ya makanisa kuhuisha wito wao wa pamoja kutafuta kuwa na ushirika *(koinonia)* ambao ni Karama na ahadi ya Mungu, ili kuimarisha huduma yao *(diakonia)* kwa watu na ulimwengu na uumbaji, kujizatiti wao wenyewe kwa utume wa Mungu wa upendo kwa ulimwengu *(missio Dei)*, na kuweka maneno kwenye ombi lao la pamoja kwa ajili ya kila mtu na kwa ulimwengu mzima *(leiturgia)*.

Ujumbe uliopangwa kwa ajili ya mkutano wa mwaka 2022 mjini Karlsrune unatukumbusha kwamba kanisa, kama mwili wa Kristo, linaongozwa na Kristo mwenyewe, ambaye upendo wake kwa ulimwengu, ambao ndio upendo wa Mungu, ulikuwa wa juu sana hadi akajitoa na hata kufa kwa ajili yake. Tunapoongozwa na kile ambacho kimefunuliwa na kutolewa kupitia upendo wa Kristo, hivyo tumepewa karama ya Kristo mwenye upendo, kupitia kwake, vyote ambavyo Mungu aliviumba. Kuwa “katika Kristo,” hatuongozwi tu na upendo bali tumebarikiwa kwa karama ya upendo. Katika 2 Wakorintho, Paulo analiambia kanisa la awali kwamba “upendo wa Kristo watubidisha.”

Ujumbe wa injili na mafungu mengi katika Agano Jipya lote, mafungu mengi kati yake yataangaliwa katika mkutano, hutuonesha jinsi ambavyo upendo wa Mungu ulivyofunuliwa katika Yesu Kristo ulishuhudiwa kwa mara ya kwanza na kutafsiriwa na kanisa la awali. Fungu kuu ni Mathayo 9:35-36, linaloelezea upendo wa Kristo, uliofunuliwa na kutendwa katika huduma yake unafananaje. Tunasoma kwamba



Picha: Albin Hillert/WCC

*Yesu akazunguka katika miji yote na vijiji vyote, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri habari njema za Ufalme, na akiponya kila ugonjwa na kila aina ya maradhi. Alipoona makutano, aliwahurumia kwa sababu walikuwa wanasumbuka bila msaada, kama kondoo wasiokuwa na mchungaji.*

Tunaona katika mafungu haya Kristo ambaye aliwahurumia, akiguswa kwa kina “katika hisia zake”, yeye anayeleta habari njema, uponyaji na tumaini kwa wale ambao “wanasumbuka bila msaada.” Upendo wake si tu kwa ajili ya wanafunzi wake pekee, bali ni kwa ajili ya kusanyiko lote, kwa wale waishio mijini na vijijini ambao walikusanyika nyikani ili wasikilize mafundisho yake na kwa wale wote ambao Mungu amewaumba.

Upendo huu si tu upendo wa mwandamu aliyejawa Roho Mtakatifu bali ni upendo wa Mungu ndani yake na kupitia yeye. Upendo huu wa Mungu ni mpana sana, wa kina ukileta tumaini la kweli na linalobadilisha maisha. Ni aina hii ya upendo, upendo wa yule ambaye Mungu anakaa duniani katika hali yake yote ya majeraha na kuvunjika, ambao unaongoza kanisa na daunia.

Mkutano huu utatoa fursa ya kutafakari kwa kina maana ya upendo wa Kristo, na kujikuta sisi wenyewe na upendo ambao sisi sote tunaupokea na kuutoa, umefanywa upya na kuhuishwa kupitia Kristo kututazama kwa upendo. Tutagundua pamoja vile ambavyo upendo si tu (kama ambavyo unafasiliwa mara nyingi) hisia za kimihemko au kimapenzi bali unaweza kuwa ushiriki katika upendo wa Mungu uliodhihirishwa kwa Kristo: upendo unaokomboa, unaojikana nafsi, na wa kujitoa dhabihu na unatenda kazi katika kuleta mabadiliko kwa ajili ya mema.

## *“ . . . unauleta ulimwengu katika umoja na upatanisho “*

### *Kushughulikia changamoto za nyakati zetu kwa kusukumwa na upendo wa Kristo*

Mkutano wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni ni mahali ambapo tunakusanyika kama ushirika kutoka duniani kote, na vilio na mahitaji ya ulimwengu yanayoletwa na washiriki na wajumbe wote wa mkutano. Kama makanisa, sisi ni ishara ya ulimwengu wa ufalme wa Mungu ujao: tunatafuta ufumbuzi wa dhati wa changamoto nyingi za wakati wetu na kuwa mitume ambao kwa maisha yetu tunaubadilisha ulimwengu.

Lakini tutasema nini kuhusu ulimwengu ambao unasukumwa na upendo wa Kristo? Ni kitu gani katika maisha ya ulimwengu, nyakati hizi, ambacho kinatoa changamoto kwa imani yetu, ushuhuda wetu na jitihada zetu kwa ajili ya umoja wa Wakristo na umoja wa wanadamu na uumbaji wote?



Picha: Albin Hillert/WCC


Picha: Marcelo Schneider/WCC


Picha: Mike DuBose/United Methodist News Service


Picha: Mike DuBose/United Methodist News Service

## Uviko-19

Ulimwengu mzima umepata uzoefu wa kukabiliana na janga la dunia. Watu wengi sana walikufa na kwa watu walio wengi zaidi Uviko-19 umeleta majonzi, udhaifu na wasiwasi mkubwa juu ya mstakabali wa maisha yajayo.

Huu ni wakati uliopotea ambao ulitupigisha magoti umetufanya tuwe wanyenyekevu, huku watu na jumuiya nyingi wakipitia mfadhaiko mkubwa, huku baadhi yao wakiwa na mfadhaiko mkubwa sana kiasi cha kutamani kutoa uhai wao.

Tumenyenyekezwa na matukio haya. Yametudhihirishia ni kwa kiasi gani tunahitaji uhusiano wa kila mmoja hata kwa muda, pamoja na masharti ya kujitenga ili kuzuia maambukizi,. Watu wote wanahitaji upendo na msaada, lakini upendo unakuwa mgumu kuelezwa na kufanywa uwe dhahiri katika nyakati hizo.

Vilevile Uviko-19 umedhihirisha  wazi namna ambavyo dhana ya kujitosheleza, kujitegemea na dhana ya kuwa mtu huru ambayo ni maisha ya watu wengi hususan katika nchi za Magharibi, ni mambo ya kufikirika tu. Imeonesha dhahiri kwamba sisi binadamu si watawala wa uumbaji bali ni sehemu ya uumbaji na tunaweza kukabiliwa na hatari ndani yake.

Janga hili pia limedhihirisha hali kubwa ya kutokuwa na usawa duniani na limeongeza uzito wa ufahamu wetu kuhusu changamoto kubwa zaidi za nyakati zetu. Makanisa pia, yamehangaika kujua namna ya kuendelea katika ibada, kusherehekea sakramenti, na katika kuihudumia dunia, na wakati mwingine wamekuwa na bidii ndani yao wenyewe au kuyasisitiza mamlaka kuhusu vile wanavyopaswa kuwa waaminifu kwa Mungu na watu wa Mungu.

Dunia inasikika kwa vilio vingi vya maumivu, mateso na maandamano kutoka katika jumuiya na watu vilevile kutoka katika uumbaji wenyewe. Duniani kote watu “wanasumbuka bila msaada, kama kondoo wasio na mchungaji.” Na kwa watu wote wa duniani, hasa kwa watu masikini ambao wanateseka sana, kama kawaida, Kristo anawahurumia.

# Mabadiliko ya tabianchi

Tunaishi katika ulimwengu ambapo tabianchi inabadilika, inabadilika kwa sababu ya kile ambacho binadamu wamefanya.

Dunia, ambapo ni makazi yetu inateseka kwa sababu ya wanadamu. Watu wengi, hasa vijana, sasa wanazungumza kuhusu hali ya dharura ya tabianchi. Kuanzia kwenye kilele cha mlima Everest (taka) hadi kwenye kina cha bahari (plastiki), kuanzia Siberia (halijoto ya juu) hadi mlima Kilimanjaro (theluji yake "ya milele" inatoweka) na katika Bahari ya  Pacific visiwa (vingi huenda vitazama), ishara muhimu za sayari zinaonyesha madhara ya maisha ambayo watu wengi wameyaishi. Viumbe vingi sasa vinakabiliwa na tishio la kutoweka, na bioanuai kubwa ya viumbe, ambavyo sote tunavitegemea vinatishiwa vikali. Tumejifunza kwamba maisha bila mipaka yanaleta uharibifu bila mipaka.

Kwa wanasayansi wengi, dunia leo ipo katika kipindi kipya cha historia yake, inayoitwa Antroposini, ambapo athari ya utawala wa wanadamu, hususan katika kipindi cha miaka 200 iliyopita ya mapinduzi ya viwanda, hayawezi kubadilishwa tena. Wanadamu wameshindwa kulinda viumbe na sasa upendo wa Mungu kwa viumbe wote, uliodhihirishwa katika Kristo, unatoa wito kwa ajili ya mabadiliko na kwa ajili ya kuungama kwetu. Hata hivyo, kama wale walio katika Kristo, ambao ni malimbuko ya uumbaji mpya (katika dunia kufanya upya), tuna tumaini lisilopingwa kwa ajili ya wakati ujao.


Picha: Sean Hawkey/WCC



Picha: Marcelo Schneider/WCC



Picha: Marcelo Schneider/WCC



Picha: Sean Hawkey/WCC



## Kukosekana Usawa

Ulimwengu tunamoishi hivi sasa unatawaliwa na mfumo wa uchumi ambao unalimbikiza mali kwenye mikono ya watu wachache na kuzidisha kutokuwepo usawa baina ya mataifa na baina ya makundi ya jamii ndani ya taifa. Hali kama hizo za kutokuwa na usawa zimezidishwa na kuimarishwa na janga hili la Uviko-19. Katika baadhi ya maeneo, nchi zilielekea kufa kiuchumi, tangu waanze kukabiliana na janga hili, pamoja na hili, changamoto nyingi zinaonekana kuwa ni pigo la mwisho. Baadhi ya mataifa yalifikia hatua ya kujaribu kujitegemea wenyewe kiasi cha kutaka kujiondoa katika makubaliano ya mashirikiano na misaada ya kimataifa wakidai kuwa ni bora "kujilisha sisi wenyewe."

Hali halisi ilivyo duniani kote inapingana na utamaduni wa kibiblia wa huruma kwa yatima, mjane na mgeni kama ishara ya uaminifu kwa agano la Mungu kwa watu wake, utamaduni uliowekwa ndani ya huruma ya Yesu kwa wale wanaoishi "katika ukingo" kama kondoo wasio na mchungaji. Katika miaka ya hivi karibuni, makanisa mengi na mashirika ya kitume yamekuwa yakitoa wito kubadili mfumo wa "uchumi mpya wa maisha" kupitia mfumo mpya wa kimataifa wa uchumi na fedha.

Pia tumekuwa mashahidi wa ukatili wa kutisha na tumeshuhudia maandamano makubwa dhidi ya ukosefu wa usawa ambayo wazungu wanaitegemeza na ubaguzi unaongezeka nguvu, wakati ulimwengu unasikia sauti za kinabii zinazotangaza kwamba "Maisha ya Watu Wesusi ni Muhimu."

Katika ujumbe wake uliorekodiwa kwa wajumbe wa mkutano wa saba wa kila mwaka wa Jukwaa la Imani Anuai la G20, Mzee wa Ekumeni Bartholomew I, alisisitiza, kuhusiana na harakati za "Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu" (Black Lives Matter), kwamba *"kila mwanadamu amepewa thamani na Mungu isiyo na kikomo. . . haiwezi kupunguzwa kuendana na thamani ya soko, kwa ajili tu ya kubadilishana na bidhaa."* Pia alionesha kwamba *"utu wa binadamu hauna rangi, jinsia, umri, mbari au dini. Kila mtu ana thamani sawa, kwa hivyo kuheshimiwa na kutendewa kwa usawa kwa binadamu kunapaswa kufanywa kila wakati na kila mahali. . . Tungependa kutumia fursa hii ili kupaza sautu yetu dhidi ya uonevu wa kimfumo, aina yoyote ya ya ubaguzi wa rangi, ubaguzi wa kikabila, ukabila na matabaka. Watunga sera na wale wanaotekeleza sera wanapaswa kujua kwamba tunataka kila mtu asivumilie uonevu na aina yoyote ile ya vitendo vya kibaguzi."*[2]

2 Kama ilivyoripotiwa na https://www.romfea.gr/oikoumeniko-patriarxeio/39899-oikoumenikos-patriarxis-kaloume-se-mideniki-anoxi-apenanti-stin-adikia.



Picha: Marcelo Schneider/WCC



Picha: Albin Hillert/WCC

## Mapinduzi ya Kidijitali

Mapinduzi ya teknolojia ya kidijitali yanayotawala duniani yanaweza kuwa na madhara makubwa kuliko yaliyofanywa na zama za mapinduzi ya viwanda. Yanabadilisha kwa kasi ya juu kwa jinsi tunavyoishi, kufanya kazi na kuhusiana na wengine. Inakidhi vizuri baadhi ya mahitaji ya watu ambao hawawezi tena kukutana ana kwa ana, inawezesha mawasiliano na kufanya kazi kuvuka mipaka, lakini pia inaibua maswali ya kina ambayo si mazuri kuhusu uelewa wetu wa kile kinachomaanisha kuwa binadamu.

Harakati za kuachana na mawasiliano ya ana kwa ana, katika hali fulani, yanaweza kusababisha aina mpya ya kutokuwa na uhusiano miongoni mwetu. Hapo baadaye tunaweza kujikuta tunashinda vikwazo vya kibinadamu vya kiakili na kimwili kiasi kwamba kile tunachomaanisha "binadamu" leo kinaweza kisiendane na kile ambacho neno "binadamu" linamanisha wakati huo. Akili bandia, alogarithimu, kompyuta kufanya shughuli za kibinadamu, tafiti za kibiolojia ili kuunda wanadamu ambao ni "wakamilifu" zaidi, utengenezaji na matumizi ya roboti, haya yote yanaibua maswali mapya kuhusu uhuru na utambulisho.



Picha: Albin Hillert/WCC



Picha: Marcelo Schneider/WCC



Picha: Albin Hillert/WCC

## Kupotea kwa imani na tumaini juu ya uwezekano wa maisha bora yajayo

Katika ulimwengu ambao watu wengi wamepoteza imani juu ya  serikali zao, mashirika ya kimataifa, au katika ushirika na ambapo watu wengi wameona mmomonyoko wa haki na uhuru wa binadamu, kuna haja ya kufufuliwa tumaini na njozi kwa ajili ya maisha yajayo. Miaka ya hivi karibuni limeshuhudiwa badiliko la dunia na kuwa na mtazamo wa kujiangalia na kutengana badala ya kuwa na umoja wa eneo husika badala ya jumuia za kimataifa na thamani kubwa imewekwa kwenye tofauti na utambulisho wa ndani ya nchi kuliko umoja wa binadamu wote.

Ulimwengu unagugumia kwa maumivu kwa sababu kuna migogoro baina ya nchi na nchi, kwa sababu kuna wakimbizi wengi na watu wasio na makazi au watu walioteswa:  kwa sababu wanawake na  watoto wanakabiliana na ukatili na kwa sababu watu wengi wana njaa na wapo hatarini na wanaogopa.  Kabla ya mateso makubwa na uonevu, serikali za dunia na mashirika yanaonekana kuwa na mchango mdogo sana pia huweza sehemu wanaoimarisha mateso na madhila mengi.

Lakini katika maeneo mengi janga la ugonjwa, limeamsha mshikamano ambapo jirani hufanya kazi na jirani kupata ufumbuzi wa tatizo jambo linalogusa nyoyo: majirani wanawasaidia majirani, wakati serikali na mashirika ya afya yanafanya kazi pamoja ili kuleta unafuu, wakati wanasayansi wanafanya kazi kutafuta na kujaribu chanjo na kadiri mataifa yanavyofanya kazi pamoja kama mataifa. Kuna ishara ambazo dunia inazihitaji, na wanazilililia, dhana mpya ya umoja na tumaini. Kuna wale wanaotafuta njia za kufanya upendo uwe halisi na dhahiri katika jukwaa la umma, upendo ambao umeimarisha maisha yetu yote binafsi na ya faragha. Tunaishi katika ulimwengu ambao linapokuja suala la hayo mambo kama vile mabadiliko ya tabianchi, umasikini na afya, tunakuwa wamoja. Janga hili limefanya ukweli huu uwe dhahiri kabisa.


Picha: Albin Hillert/WCC


Picha: Presbyterian Church in the Republic of Korea



Foto: Marcelo Schneider/WCC



Foto: Albin Hillert/WCC

## Ulimwengu unalilia Haki na Amani

Dunia tunamoishi, na ambamo mkutano wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni litakutana mwaka 2022, imechafuliwa na aina nyingi za uonevu na kwa maumivu ya watu wake wengi, viumbe wake, na hata dunia yenyewe. Kuna vita na vurugu za kutisha kwenye maeneo mengi, wakati mwingine, majanga, na mengine yakianzishwa kwa jina la dini, huku watu wakiendelea kuomba na wakitamani amani. Kuna hali mbaya ya kutokuwa na usawa, wakati watu wachache wanafanya karamu wengine wanakufa kwa njaa. Kuna njia nyingi ambazo wanadamu wanaendelea kuwatawala wengine, kuimarisha kiburi na kuonesha nguvu ya kuwatenga wengine na kuwanyonya. Rasilimali za uumbaji zinaendelea kunyonywa na kutumiwa vibaya, wakati kutubu na kufanywa upya kunahitajika kutoka kwetu sote ambao tunashiriki makazi haya ya pamoja.

# Mtazamo wa kwanza kabisa wa Mungu kwa ulimwengu: Upendo

Lakini katika nyakati kama hizi, kama wale ambao wapo katika Kristo, hatujaachwa bila tumaini, hata tunapokabiliwa na changamoto kubwa hizo. Hakika, tuna karama na baraka hizo kutoka kwa Mungu kwamba tunajua hatuhangaiki peke yetu na kwamba hatuna rasilimali zetu pekee za kuzitegemea. Mungu anafanya kazi duniani na ndani ya watoto wa Mungu kanisani. Andiko la WCC kuhusu Kanisa na Utaratibu wa Imani,: Kuelekea katika Njozi Moja, katika sura yake ya mwisho, hutukumbusha kwamba

*Mtazamo wa wa kwanza kabisa wa Mungu kuhusu ulimwengu ni upendo, kwa kila mtoto, kwa kila mwanamke na mwanaume ambaye amekuwa sehemu ya historia ya mwanadamu, na kwa uumbaji wote.*[3]

“Mtazamo wa kwanza wa Mungu” umefanywa mwili katika Yesu Kristo: katika huruma aliyoionyesha kwenye huduma ya kidunia; katika fumbo la kufanyika kwake mwili; katika mateso yake, kifo na kufufuliwa tena katika maisha mapya; na katika ahadi ya ulimwengu ujao kufanywa kuwa mpya. Na upendo huu, upendo ambao alipenda na upendo uliowezekana ndani yetu, ni karama ya Mungu katika kanisa na kwa ulimwengu. Ni upendo huu ambao unahamasisha, unatoa msukumo na unaunda yote ambayo yanawezekana katika uhai wa kanisa kadiri linavyokuwa ishara ya upendo wa Mungu kwa ulimwengu.

Ujumbe wa mkutano huu hautaji waziwazi kanisa na huachwa wazi jinsi ambavyo upendo wa Kristo unaweza kudhihirika ili kwamba ulimwengu uguswe. Kanisa linaweza kuhitaji kuwa na uadilifu fulani, kwa kuwa si watu wake wote na katika kila namna wanadhihirisha upendo wa kina wa Mungu. Lakini kanisa linaweza kufurahi kwamba, kwa mpango wa Mungu, ni uumbaji mpya, ishara na mtumishi wa utume wa Mungu duniani, na utume huu daima unatokana na upendo, unaoonyeshwa katika imani iliyotangazwa na mitume.



Foto: Albin Hillert/WCC

---

3 Kama ilivyoripotiwa na https://www.romfea.gr/oikoumeniko-patriarxeio/39899-oikoumenikos-patriarxis-kaloume-se-mideniki-anoxi-apenanti-stin-adikia



Picha: Geoffrey Alemba/WCC




Maisha ya kanisa katika ibada yake na huduma kwa ulimwengu, imeitwa kuwa ishara ya upendo uliodhihirishwa katika Kristo na kudhihirishwa katika maisha na mitume kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu. Huu ni upendo ambao unaweza kuubadilisha ulimwengu kuwa na upatanisho na umoja. Umoja wa kanisa, kama mashuhuda wa upatanisho, unapaswa pia kutambulishwa na kuhusianishwa na huduma katika dunia na mabadiliko ya ulimwengu. Ujumbe wa WCC wa hapo awali, *Kanisa na Dunia,* ulielezea kama hivi:

*Katika kutoa maisha yake ya kawaida katika huduma ya Mungu na upendo wa Mungu kwa ajili ya dunia, kanisa pia limeendelea kupambana kupitia uwepo wake pamoja na wale ambao wanateseka kwa matendo yao kwa niaba yake. Katika kushiriki upendo huu wa Mungu kanisa linawawezesha kuelewa upendo wa Mungu unaovumilia katika Yesu Kristo kwa ajili yao, na kanisa lenyewe linaongozwa katika uzoefu wa kina wa upendo huo.*[4]

Ni upendo huu ndio unaowahamasisha wale ambao wanamfuata Kristo kuwa karibu na kila mtu katika umoja ambao ni karama ya Mungu. Upendo huhamasisha ushirika na upendo hutuweka pamoja. Kristo mwenyewe kwa kuipenda Yerusalemu, alilia,

*"Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako pamoja, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake, lakini hukutaka!" (Luka 13:34)*

Upendo, zaidi ya mawazo na uwezekano, hukusanya, huhamasisha na huunda umoja. Kanisa ni ishara ya upendo huu wa kujikana nafsi wa Kristo ulimwenguni, na watu wa kanisa ni watumishi wa injili ili kwamba kupitia upendo wao, katika mtazamo na vitendo, wanaweza kuhamasisha matendo hayo nje ya kuta za kanisa. Ushuhuda huu hautokani na jitihada za wanadamu pekee na hautokani na mitazamo ya kimahaba na ya ufahamu mdogo wa matamanio ya kibinadamu lakini hufanywa kwa upendo wa Kristo unaofanya kazi ndani yetu.

Kristo, kwa upendo, aliomba kwa ajili ya umoja wa rafiki zake na wanafunzi (Yohana 17). Aliomba "ili wawe wamoja kabisa," si kwa ajili yao tu bali pia ili kwamba ulimwengu uweze kuamini. Kile ambacho kanisa linatarajiwa kuwa na kile ambacho kanisa linapaswa kuwa ni pande mbili za sarafu moja. Kanisa ni moja, kulingana na maandiko na imani ya kitume pia limeitwa kuwa ishara ya umoja kwa ajili ya ulimwengu uliogawanyika.

4 *Kanisa na Ulimwengu*, Makala ya Imani na Utaratibu 151, §38 (Geneva: Machapisho ya WCC, 1990), https://archive.org/details/wccfops2.158/page/32/ mode/2up.



Picha: Marcelo Schneider/WCC


Picha: Geoffrey Alemba/WCC

Kutoka katika moyo wa Kristo mwenye upendo linatoka ombi kwa ajili ya umoja. Katika ibada ya kikristo, ekaristi inaonesha uhalisia wa upendo wa Mungu uliodhihirishwa kwa Kristo kupitia kufanyika mwili, msalaba na ufufuo. Ni upendo huu ndio unawasukuma wafuasi wa Kristo si tu kupendana wao kwa wao, lakini pia kwa ajili ya ulimwengu alioufia. Kristo anawagusa watu wake waonyeshe upendo kwa ajili ya ulimwengu ambao aliufia na kuwa ishara ya uponyaji, upatanisho, na umoja ambao ulimwengu iliovunjika unalilia.

Ushahidi wa mitume ni kwamba Kristo anavunja alama zote zinazofahamika za toafuti na mgawanyiko.

*Wala hakuna tena Myahudi au Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume wala mwanamke, maana nyote mmekuwa wamoja ndani ya Kristo Yesu. (Gal. 3:28)*

Kanisa linashuhudia upendo wa Mungu anayependa, anayependwa, ambaye ni pendo.[5] Kanisa linashiriki katika umoja wa kwenye moyo wa Mungu na linajitoa kama ishara ya eskatolojia na mtumishi wa umoja wa uumbaji wa Mungu hutimizwa na kuukuza. Kwa hiyo, umoja tunaoutafuta si tu mradi wa pamoja kulingana na matamianio ya pamoja bali umejengwa katika upendo wa Mungu unaotuleta pamoja na unaotuunganisha.

Ni sababu ya maombolezo ambayo utengano wetu wa sasa, kukosa upendo sisi kwa sisi, na hitaji letu la kuweza kupatanishwa, wakati mwingine katika kanisa hutufanya tuonekane kuwa ishara na mtumishi mbaya wa Kristo ambaye anatuita tuwe wamoja, lakini hii ni changamoto iliyopo mbele ya kanisa na ahadi ya tumaini pia.

Makanisa yatakapokuwa na umoja, yanafanya hivyo tu kama mashahidi kwa ulimwengu lakini kama sehemu ya ulimwengu ambao Mungu ameuumba.

Tayari, ndani ya kanisa lenyewe, dunia inakusanywa pamoja. Kama ambavyo jarida la *Kanisa na Ulimwengu* linavyoelezea,

*Kinachokusanywa, kupatanishwa na kuhuishwa ni kanisa, kwa kweli, "dunia" katika kutengana kwake na Mungu na hivyo mchakato huu wa kuhusihwa unaendelea kurejelea nyuma katika dunia na mbele katika katika ukombozi wake wa mwisho.*[6]

Upendo wa Kristo, pamoja na kwamba unaleta umoja kanisani, unauleta ulimwengu katika upatanisho na umoja.

---

5 Fikra dhanifu kuhusu pendekezo lililofanywa na Augustine, kulingana na tamaduni za Magharibi, katika kazi yake *De Trinitate.*

6 *Kanisa na Ulimwengu*, §14.


World Council of Churches
GETI 2018
World Council of Churches



Picha: Albin Hillert/WCC

## Ushirika (Ekumeni) wa Moyoni

Hii ni mara ya kwanza ambapo neno “upendo” limekuwa sehemu ya ujumbe wa mkutano wa WCC. Linaweza kuwa linamaanisha nini kwa ajili ya harakati ya kiekukmeni ili kujengwa na moyo vilevile na kichwa, kuishi kwa kuiga mtazamo wa Mungu wa kwanza kabisa kuhusu ulimwengu, upendo wenyewe?

Watu wengi katika makanisa wanasisitiza kwamba kazi yetu ya kutafuta umoja isiwe ya kiakili tu, kitaasisi, na kazi rasmi, bali vilevile ijikite katika uhusiano, katika ombi la pamoja na zaidi ya yote, katika kupendana na kujaliana. Inapaswa pia itokane na imani ya mitume, ya wale ambao walipewa amri mpya ya “kupendana ninyi kwa ninyi,” wakati Kristo ambaye aliwaita marafiki (na si watumwa) aliwatawadha miguu yao (Yohana 12).

Kristo huyuhyu alisisitiza kwamba “yeyote mwenye kuzijua  amri zangu na kuzishika ndiye anipendaye” (Yohana 14:21), kwa hivyo upendo si tu mihemko lakini umejengwa katika uaminifu uanafunzi unaobadilisha.

Kama wanadamu, tunajua vizuri sana kwamba umoja na upendo hukaa pamoja. Neno lenyewe “ushirika” (koinonia), neno ambalo tunalichagua mara nyingi kuliko neno “umoja”, humaanisha aina ya umoja ambayo inatokea watu wanapopendana. Katika maisha yetu ya uhusiano wa kina zaidi tunaweza, ikiwa tumebarikiwa kweli na kama ni shughuli yetu, kupitia uzoefu wa maajabu ya aina ya upendo ambao unawaleta wanadamu pamoja kwa namna ambayo wanafanywa kuwa wamoja, si tu kimwili bali tunaweza kusema, kiroho pia. Na kuna mahusiano mengi katika maisha yetu, ambayo tunajua umoja na uhusiano unaweza kuwa karibu kiasi gani.



Picha: Albin Hillert/WCC



Picha: Albin Hillert/WCC

Upendo unatuunganisha pamoja, unatuafanya tutake kukaa pamoja, kushiriki kila kitu tulichonacho, kujenga jumuiya mpya, kuleta uhai na kusimama pembeni ya kila mmoja na wakati ambapo matatizo yanakuja na mateso yamekuwa makali.. Upendo na ushirika huenda pamoja. Umoja na upendo huenda pamoja. Upendo hutuleta katika umoja.

Kuweka mkazo kwenye upendo si tu unatuleta pamoja kama Wakristo lakini pia hutuleta katika uhusiano wa kina pamoja na watu wote wa imani na watu wote wenye nia njema. Upendo kama ujumbe unaotiririka katika tamaduni tofautitofauti za imani umeleta msingi imara kwa ajili ya huduma na kutafuta haki ambayo inavuka mipaka. Katika upendo tunavuta umakini si tu kwetu lakini pia kwa “wengine,” kuwafanya majirani kuwa rafiki kwa kufanya ukarimu mkubwa na kuwa na umoja. Upendo kama lugha ya imani unaweza kuuhusisha ulimwengu kiutendaji na kinabii kadiri tunavyoona na kuuhisi leo kwa namna ambayo italeta tofauti kwa ajili ya kesho ya pamoja.

Uwepo wetu kama Wakristo katika ulimwengu wenye dini nyingi hutuita kuiishi amri ya Yesu kuwapenda majirani kwa kushikilia imani ambayo inatoka moja kwa moja katika kujitolea kikamilifu na kutaka sana kukuza mjadala huu. Kutokana na makala ya *Kuuhudumia Ulimwengu uliojeruhiwa katika Umoja wa Dini*: *Wito wa Kikristo Kutafakari na Kuchukua Hatua Wakati wa Uviko-19 na Zaidi*, ambayo iliandikwa kwa pamoja na WCC na Baraza la Maaskofu kwa ajili ya Mjadala wa Dini, hutukumbusha:

*Imani yetu inakuwa hai katika vitendo vinavyoongozwa na upendo wa Kristo. . . Huiweka imani yetu na utume kuwa hai na kamilifu. huongoza maisha yetu kama Wakristo kuwa ishara njema ya uwepo wa Kristo, na hujenga*

*upendo na maelewano kati yetu na wale ambao tunajiunga nao ili kudhihirisha upendo wetu katika vitendo.*[7]

Tunajifunza pia, kwamba upendo ni zaidi ya mihemko na hisia, kwamba unapimwa kadiri ya muda unavyokwenda na unahusu kujizatiti nia na akili vilevile udhihirishaji wa hisia. Upendo ni kitu ambacho Kristo anatuamuru; si kitu ambacho kinaweza "kuibuka" tu. Kinahusu siasa zetu, vitendo vyetu, na kutafakari kwetu kwa makini kuhusu hisia zetu. Ni, kama Mtakatifu Paulo alivyowaandikia Wakorintho (1 Kor. 13:1-7, 13), huvumilia, upendo hufadhili, hautaki mambo yake yenyewe, hauweki kumbukumbu ya mabaya, hufurahi pamoja na kweli. Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote.

Katika safari ya kuwa na umoja wa Kikristo, wakati fulani tumedhani kwamba tutakapojijua kwamba tumeunganika kabisa, wakati ambapo siku hiyo itakuja, basi tutaweza kupendana kikamilifu. Tutakapojua kwamba tuna imani moja ya kitume, tunapoweza kutambua ndani ya kila mmoja wetu, kanisa moja, takatifu. majumui na la kitume, tunapoweza kukusanyika katika meza moja, basi tutaweza kupendana.

Lakini hadi wakati huo, pengine ushirika wetu utawezekana, na tutaongozwa kuupokea tunapoanza kupendana, si tu kinadharia au kidhahania bali kwa namna ambayo inaonekana na kutafakrika iliyofanywa kuwepo, kwamba kila mtu anayetutazama aweze kuona. Hii kwa kweli inaweza kuwa ushirika (ekumeni) ya moyoni.



Picha: Albin Hillert/WCC



Picha: Albin Hillert/WCC

7 Baraza la Makanisa la Ulimwengu na Baraza la Maaskofu kwa ajili ya Mjadala wa Dini, *Kuuhudumia Ulimwengu Uliojeruhiwa katika Umoja wa Dini: Wito wa Kikristo katika Kutafakari na Kuchukua Hatua wakati wa Uviko-19 na Zaidi* (WCC na PCID, 2020), 17, https://www.oikoumene.org/resources/ publications/serving-a-wounded-world-in-interreligious- solidarity.




Picha: Albin Hillert/WCC

# Hitimisho

Harakati ya Ushirika (kiekumeni) daima imekuwa inayohusu makanisa yakihamasishana kuwa na umoja unaoonekana, kuwa na ushirika mkamilifu. Leo, kwa sababu ya janga la ugonjwa hata kukutana ana kwa ana limekuwa jambo gumu sana, kiasi kwamba wito unahitajika zaidi.

Kwa sasa makanisa yanahitaji sasa, *pamoja,* katika harakati za kiekumeni zilizohuishwa kwa ajili ya dunia ili kupata sauti ambayo ni ya umma zaidi kwa ajili ya kuzungumza tumaini la kweli zaidi kuliko matumaini hewa ya ahadi za kisiasa: tumaini ambalo linaweza kuijenga dunia bora kuliko ile ambayo imekitwa kwa kina zaidi na mali, hali ya kujitosheleza na harakati za kujali maslahi ya watumiaji wa bidhaa, dunia ambapo nyenzo zitatumiwa pamoja, hali ya kutokuwa na usawa imeshughulikiwa na utu mpya umepatikana baina yetu na kwa ajili yetu sote.

Makanisa ambayo yanaishi na kusali wakiwa mafichoni, jumuiya za faragha, zikiwa zimejitenga kutoka kwa wengine, zinaitwa na Kristo aliyefufuka “waende” kwa watu na kufungua nafasi za dunia, kufasili upya mambo yaliyo muhimu kwetu, kuangusha sanamu na kuwa sehemu ya kukaribisha ufalme wa Mungu ambao masikini wanabarikiwa na wafungwa wanaachwa huru. Ulimwengu unaolilia upendo wa kina, kwa ajili ya jumuiya, kwa ajili ya haki na tumaini huhitaji makanisa ambayo yanaonekana katika ushirika, wakihitaji umoja palipo na utengano kutafuta kesho mpya kwa ajili wanadamu na kwa ajili ya uumbaji wote, kama ilivyoelezwa katika Ufunuo 21.

*Upendo wa Kristo Unaileta Dunia katika Upatanisho na Umoja.* Ujumbe wa Mkutano wa 11 ni wimbo wa sifa kwa Mungu ambaye upendo wake, katika Kristo hutuhamasisha. Ni kauli ya *imani na kutumainia* ambayo ni mapenzi ya Mungu kutuongoza kwa upendo kuwa na upatanisho na umoja. Ni ujumbe kwa ulimwengu kuhusu upendo ambao ni moyo wa imani ya Kikristo. Ni mwaliko kwa makanisa na kwa wote wenye nia njema duniani kote kushiriki katika hekima ya kawaida ya upendo ili kutuongoza sote kupata upatanisho na kupata umoja wetu wa kweli kama wanadamu.




**World Council of Churches**


Anwani ya Posta:
S. L P 2100
CH-1211 Geneva 2
Uswisi

Anwani ya eneo:
150 Route de Ferney
Grand-Saconnex (Geneva)
Uswisi

Simu: (+41 22) 791 6111
Nukushi: (+41 22) 791 0361

www.oikoumene.org

worldcouncilofchurches @oikoumene @worldcouncilofchurches wccworld



"Upendo wa Kristo unaileta Dunia katika upatanisho na umoja" tafakuri juu ya ujumbe wa Mkutano wa 11 wa Baraza la Makanisa la Ulimwengu, Timu ya Uzalishaji ya Karlsruhe 2022: Odair Pedroso Mateus, Marianne Ejdersten, Stephen Brown, Marcelo Schneider, Krystyna Konovalova Mbunifu: Juliana Schuch Jalada la Juu: Imetokana na ishara ya Mkutano wa 11 wa WCC Picha ya jalada la nyuma: Albin Hillert/WCC



9 782825 417560